TANGAZO LA SERIKALI NA. 439 la Tarehe 31/5/2024

SHERIA YA SERIKALI ZA MITAA (MAMLAKA ZA WILAYA),
SURA YA 287

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 153(1))*

MAREKEBISHO YA SHERIA NDOGO YA UDHIBITI NA USIMAMIZI WA MIFUGO YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MOSHI, 2024

Jina

TS Na 38 ya 2024

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Marekebisho ya Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2024, na itasomwa kwa pamoja na Sheria Ndogo ya Udhibiti na Usimamizi wa Mifugo ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ya Mwaka 2024 ambayo hapa imerejewa kama "Sheria Ndogo Kuu".

Marekebisho ya aya cha 3

2. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa kwenye aya ya 3 kwa-

(a) kufuta maneno "binafsi" katika tafsiri ya msamiati "mfugo"; na

(b) kuongeza maneno "Halmashauri ya" kabla ya maneno "Wilaya" katika tafsiri ya msamiati "Mkurugenzi".

Marekebisho ya aya cha 10

3. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 10 kwa kufuta aya ndogo ya (4) na kuandika upya kama ifuatavyo:

"(4) Bila kuathiri masharti yaliyowekwa katika aya ndogo ya (3), kabla ya kuuza mfugo uliokamatwa kwa mnada, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mmiliki na umma juu ya kusudio la kuuza mfugo huo".

Marekebisho ya aya ya 22

4. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 22 (1) kwa kufuta maneno “hatakayeruhusiwa” na badala yake kuweka maneno “hata ruhusiwa”.

Marekebisho ya aya ya 26

5. Sheria Ndogo Kuu inarekebishwa katika aya ya 26, kwa-

(a) kufuta aya ndogo ya (s); na

(b) kubadili mpangilio wa aya ndogo za (t) hadi (v) kuwa aya (s) hadi (u) mtawalia.

Dodoma,
18 Aprili, 2024

MOHAMED OMARY MCHENGERWA
*Waziri wa Nchi- Ofisi ya Rais*
*(Tawala za Mikoa Na Serikali za Mitaa)*